Jarida La

# MIFUGO NA UVUVI

#mifugonauvuviniutajiri

TOLEO NO; WMU 0002| 2025 WWW.MIFUGOUVUVI.GO.TZ | KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

Yaliyojiri Mwezi Februari 2025



## Dkt. Samia Azindua Kampeni ya Ugawaji Boti za Kisasa za Uvuvi Awamu ya Pili - Tanga

Scan hapa Kusoma taarifa za Tovuti yetu

@Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Jarida la Mtandaoni HALIUZWI

Toleo Na.002 | 2025





# Jarida la Mtandaoni

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
Wizara ya Mifugo na Uvuvi
S.L.P 2870
Mji wa Serikali Mtumba
Dodoma , Tanzania
simu : +255 26 2322610
Barua Pepe : barua@mifugo.go.tz

@wizara ya Mifugo na Uvuvi

# Yaliyomo *Ndani* Jarida


1 TAHARIRI .............**Uk. 04**

2 Rais Dkt. Samia akabidhi boti za kisasa za uvuvi .............**Uk. 05 - 06**

3 Utambuzi wa mifugo sasa ni bure - Dkt. Kijaji .......**UK 07**

4 Bunge laridhishwa na maandalizi kampeni ya chanjo za mifugo ............. **Uk. 08**

5 Wadau wakutana kuboresha Mwongozo wa Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi ........... **Uk. 09**

6 Matukio katika picha ya ugawaji wa boti za kisasa za uvuvi awamu ya pili mkoani Tanga............ **Uk. 10**

7 Rais ameweka nguvu kukuza uchumi wa buluu - Mnyeti ...... **UK. 11**

8 Uandaaji Mitaala ya Mafunzo ya Mifugo ushirikishe wadau wa kisekta – Mhinte ........... **Uk. 12**

9 Serikali kutumia Tafiti za Kisayansi kuboresha mazao ya uvuvi baharini............. **Uk. 13**

10 Wananchi 302 wamepatiwa mafunzo ufugaji samaki kwenye vizimba Ziwa Tanganyika ............. **Uk. 14**

11 Washiriki 17 wahitimu mafunzo ya siku 14 kuongeza thamani zao la Mwani .......... **Uk. 15**

12 FETA yapokea ugeni kutoka mataifa 11 ....**Uk. 16**

13 Dkt. Kijaji ashiriki Mkutano wa Mawaziri wa Uvuvi ulioandaliwa na IOC nchini Ushelisheli ........**Uk. 16**

14 Matukio mbalimbali katika picha........... **Uk. 17 - 20**
















# TAHARIRI



UVUVI NI UTAJIRI! ndivyo ambavyo unaweza kusema kupitia Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo inahakikisha inaleta mapinduzi makubwa katika Sekta ya Uvuvi kwa kuweka jicho la kipekee kwenye Uchumi wa Buluu.

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatekeleza mradi wa ukopeshaji wa boti za kisasa kwa wavuvi wa Ukanda wa Pwani, Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa, ambapo mradi huo unalenga kuwezesha wananchi kufanya uvuvi na ukuzaji viumbe maji endelevu na wenye tija na kuwajengea mazingira wezeshi ili waweze kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi.

Makundi ya wanufaika wa mkopo huu ni wavuvi binafsi, makampuni, vyama vya ushirika na vikundi vya wavuvi na wakuzaji viumbe maji vikijumuishwa vikundi vya vijana na wanawake.

Septemba 19, 2023 Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa katika Wilaya ya Kilwa Masoko Mkoani Lindi, aliweka Jiwe la Msingi kwa ajili ya Ujenzi wa Bandari kubwa ya uvuvi kwa gharama ya Shilingi Bilioni 266 na umefika zaidi ya asilimia 79 sambamba na kuzindua Awamu ya Kwanza ya ugawaji wa boti za kisasa za uvuvi.

Wakati wa uzinduzi huo jumla ya boti 160 za mkopo wa masharti nafuu zilikopeshwa kote nchini kwa ajili ya uvuvi (boti 131) na kilimo cha mwani (boti 21) ambapo kupitia mpango huu, serikali ililenga kutengeneza ajira za moja kwa moja zipatazo 3,163 (wanaume 2155 na wanawake 1008.)

Mradi huu wa Awamu ya Kwanza ulianza Mwaka wa fedha 2022/2023 na uligharimu Shilingi Bilioni 11.5 ambapo Mhe. Rais alieleza lengo la serikali ni kufanya Mkoa wa Lindi kuwa kitovu cha Uchumi wa Buluu kwa Ukanda wa Kusini.

Kama haitoshi, Februari 26, 2025 akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Tanga, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anagonga hodi Wilaya ya Pangani kwa kuzindua Awamu ya Pili ya mradi wa kukopesha boti za kisasa za uvuvi kwa Mwaka wa fedha 2024/2025.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitenga Shilingi Billioni 14.44 kwa ajili ya kutekeleza mradi huu, hatua hii imetokana na mwitikio mkubwa wa wananchi katika kuomba mkopo huo, na hivyo kuonyesha uhitaji mkubwa, ambapo mpaka sasa jumla ya kiasi cha Shilingi Bilioni 11.5 kimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa boti 120 za kisasa na vifaa vyake ikijumuisha boti saidizi (vidingi) 118, uratibu, uhamasishaji na usimamizi wa mradi.

Katika uzinduzi huo Mhe. Rais aligawa boti 35 zilizokabidhiwa mkoani Tanga zenye thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni 4.477 na kuwataka wavuvi kuendelea kurejesha mkopo kwa wakati na kulinda rasilimali za uvuvi.

Katika uzinduzi wa mradi huu kwa awamu zote mbili, boti zimekuwa zikipokelewa kwa shangwe na wavuvi walio wengi ambapo wanasema boti moja inahudumiwa na watu kati ya 20 hadi 29 hususan vijana, zaidi ya wavuvi na jamii zao 3,163 wamenufaika na kujiongezea kipato katika awamu ya kwanza.

Wanawake pia hawako nyuma wanabainisha kuwa boti zimeongeza ushiriki wao katika shughuli za uvuvi ambapo jumla ya wanawake 1,008 wamejiunga na shughuli za uvuvi katika awamu ya kwanza.

Katika kufanikisha mradi wa mkopo wa boti za kisasa za uvuvi Wizara ya Mifugo na Uvuvi inashirikiana vyema na OR-TAMISEMI, Wizara ya Fedha, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) na Shirika la Bima la Taifa (NIC).

Kongole kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji kwa kushika vyema usukani kuiongoza wizara hii, hakika wanawake wanaweza na umeweka rekodi mpya ya kuwa waziri wa kwanza mwanamke katika wizara yetu.

Hapa ndipo tunaposema kwa herufi kubwa UVUVI NI UTAJIRI kupitia Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuipa Sekta ya Uvuvi jicho la pekee kuelekea Uchumi wa Buluu kwa kuwawezesha wavuvi vifaa vya kisasa vya uvuvi.

## Bodi ya Wahariri:

**Mwenyekiti**
**Mbaraka Kambona**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Mhariri**
**Edward Kondela** - Afisa Habari Mwandamizi

**Msanifu**
**Hamis Hussein** - Afisa Habari

**Wajumbe**
**Elibariki Mafole** - Afisa Habari Mwandamizi
**Omary Mtamike** - Afisa Habari
**Stanlay Bryaton** - Afisa Habari
**Chiku Makwai**- Afisa Habari



# Rais Dkt. Samia akabidhi Boti za kisasa za Uvuvi

## Boti 35 zenye thamani ya Bil. 4 zimekabidhiwa kwa Mkoa wa Tanga

**Na, Edward Kondela - Tanga**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewataka wanufaika wa mkopo wa boti za kisasa za uvuvi kulipa mkopo huo pamoja na kuzitunza ili mradi huo uwe na tija.


Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alibainisha hayo Februari 26, 2025 katika Wilaya ya Pangani Mkoani Tanga wakati akizindua ugawaji wa boti za mkopo kwa wavuvi awamu ya pili.

Katika hafla hiyo fupi Mhe. Rais alikabidhi boti 35 kwa wavuvi wa mkoa huo, huku akifafanua kuwa zinaendana na kuelekea katika Uchumi wa Buluu kwa kuwa zina uwezo wa kubeba samaki wengi na kufika katika uvuvi wa bahari kuu.

"Nina matumaini wavuvi wanavuna mazao mengi ya bahari kupitia boti hizo za kisasa na kupongeza ambao wameanza kulipa mkopo wa awamu ya kwanza na hatimaye kuwa na sifa ya kukopa awamu ya pili." Alisema Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya boti hizo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji, alisema boti hizo zitasaidia mbali na kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi, bali kudhibiti uvuvi haramu.

Alieleza kuwa vijana 113 wa Mkoa wa Tanga, ambao hapo awali walijihusisha na uvuvi haramu, waliamua kubadili



**Chanzo:** Idara ya Uvuvi, 2025

Endelea Ukurasa. 06 >>>

>>>Kutoka UK. 05

# Rais Dkt. Samia akabidhi Boti za kisasa za Uvuvi

maisha yao na sasa wanajiunga na vikundi vya uvuvi halali kupitia mpango huu wa mkopo nafuu.

Katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali ilitenga boti 120 kwa ajili ya wavuvi, ambapo boti 70 zitapelekwa Ukanda wa Pwani (Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Lindi, na Mtwara), boti 29 zitapelekwa Ziwa Victoria, na boti 21 zitapelekwa Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

Boti 35 zilizokabidhiwa mkoani Tanga zina thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni 4.477 na moja ya boti hizo ilikabidhiwa kwa kikundi cha vijana wa Tanga, ambao waliahidi kuwa walinzi wa rasilimali za uvuvi ndani ya taifa.

Baadhi ya wanufaika wa mradi huo ambao walizungumza na jarida hili nyakatri tofauti, walisema mkopo hupo umekuwa na tija kwao kwa kuwa boti hizo ni imara na zinaweza kukabiliana na hali yoyote ya hewa.

Aidha, wamempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan namna anavyozidi kuipa nguvu Sekta ya Uvuvi kwa kufanya shughuli zao za uvuvi kwa vifaa vya kisasa na kuomba boti zaidi ziweze kutolewa katika maeneo yote kupitia mkopo usio na riba.

Mradi huu, unaosimamiwa na Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, unalenga kusaidia wavuvi katika Ukanda wa Pwani, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa ili kuongeza tija katika Sekta ya Uvuvi na kuhakikisha uvuvi endelevu.

Awamu ya kwanza ya mradi huu ulianza Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwa gharama ya Shilingi Bilioni 11.5, ambapo boti 160 zilikopeshwa kwa wanufaika 3,163.

Huu ni mwendelezo wa juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika kuinua Sekta ya Uvuvi na kuhakikisha kuwa wavuvi wanapata nyenzo bora za kazi kwa maendeleo yao na taifa kwa ujumla, ambapo wizara inashirikiana na OR-TAMISEMI, Wizara ya Fedha, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) na Shirika la Bima la Taifa (NIC).

> *"Nina matumaini wavuvi wanavuna mazao mengi ya bahari kupitia boti hizo za kisasa na kupongeza ambao wameanza kulipa mkopo wa awamu ya kwanza na hatimaye kuwa na sifa ya kukopa awamu ya pili."*
>
> **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**
> Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania





Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji akizungumza wakati wa mkutano baina yake na Wafugaji uliofanyika Februari 19, 2025 jijini Dodoma. Kulia ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti.

# Utambuzi wa Mifugo sasa ni bure-Dkt. Kijaji

## Ni baada ya kikao na Wafugaji, Serikali yaamua kubeba gharama za Hereni

**Na, Omary Mtamike - Dodoma**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji amesema zoezi la Utambuzi wa wanyama sasa litafanyika bila gharama yoyote kutoka kwa wafugaji baada ya Serikali kuamua kugharamia zoezi hilo.

Mhe. Dkt. Kijaji alisema hayo wakati wa mkutano baina yake na wafugaji uliofanyika Februari 19, 2025 jijini Dodoma ambao ulilenga kuwahamasisha kuelekelea kwenye kampeni ya kitaifa ya chanjo naa utambuzi wa mifugo.

“Mhe. Waziri Mkuu alitoa maagizo ya kufanya tathmini ya zoezi hili na kufanyia kazi changamoto zote zilizolalamikiwa hapo awali ambapo mojawapo ilikuwa ni bei kubwa uwekaji hereni kwa mifugo na ndio maana Serikali sasa imeamua lifanyike bila gharama yoyote” Alisema Mhe. Dkt. Kijaji.

Aidha Mhe. Dkt. Kijaji alizuia ukamatwaji wa mifugo ambayo haitakuwa imefanyiwa utambuzi ambapo aliwataka watalaam wa Sekta ya Mifugo kutoa elimu kuhusu umuhimu wa zoezi hilo huku akitoa rai kwa wafugaji kutumia fursa iliyotolewa na Serikali kutambua mifugo yao.

> “*Mhe. Waziri Mkuu alitoa maagizo ya kufanya tathmini ya zoezi hili na kufanyia kazi changamoto zote zilizolalamikiwa hapo awali ambapo mojawapo ilikuwa ni bei kubwa uwekaji hereni kwa mifugo na ndio maana Serikali sasa imeamua lifanyike bila gharama yoyote.*
>
> Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji
> Waziri wa Mifugo na Uvuvi

# Bunge laridhishwa na maandalizi Kampeni ya Chanjo za Mifugo







Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti akiielezea Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo namna Wizara yake ilivyojipanga kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo za Mifugo, Februari 13, 2025 bungeni jijiji Dodoma.

**Na, Chiku Makwai - Dodoma**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo imeridhishwa na kiwango cha maandalizi kuelekea kwenye kampeni ya kitaifa ya Chanjo za Mifugo inayotarajiwa kufanyika mwaka huu 2025.

Akizungumza mara baada ya kuwasilishiwa taarifa ya maandalizi ya kampeni hiyo, Mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. Deodatus Mwanyika alisema kuwa ana imani kampeni hiyo itafanyika kwa mafanikio makubwa kutokana na namna Wizara ilivyojipanga kuitekeleza.

"Na sisi wabunge tutawasaidia kwenda kuhamasisha zoezi hilo kwa wafugaji wetu huko chini ili azma hii njema ya Serikali iweze kutekelezwa kwa mafanikio" Alisema Mhe. Mwanyika.

Akielezea mikakati ya Wizara hiyo katika kuhakikisha elimu kuhusu zoezi hilo inawafikia wafugaji wote nchini.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti alisema kuwa wizara ilishaanza utekelezaji wa mikakati hiyo ikiwa ni pamoja na kushirikisha kwa ukaribu mamlaka za serikali za mitaa ambao anaamini watawafikia wafugaji waliopo kwenye maeneo yao.

"Lakini jambo jingine chanjo hizi zitatengenezwa na viwanda vyetu vya ndani kwa sababu mbali na kuwa vina uwezo mkubwa wa kufanya hivyo tunahitaji kufanya ufuatiliaji wa karibu kwenye hatua zote za utengenezaji wa chanjo hizo ili kuwa na uhakika na usalama wake" Alisema Mhe. Mnyeti.

Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo za Mifugo inatarajiwa kufanyika kwa muda wa miezi miwili, ambapo chanjo mbalimbali za magonjwa ya ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku zinatarajiwa kutolewa.

*"Chanjo hizi zitatengenezwa na viwanda vyetu vya ndani kwa sababu mbali na kuwa vina uwezo mkubwa wa kufanya hivyo tunahitaji kufanya ufuatiliaji wa karibu kwenye hatua zote za utengenezaji wa chanjo hizo ili kuwa na uhakika na usalama wake"*

**Mhe. Alexander Mnyeti**
**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi**



# Wadau wakutana kuboresha Mwongozo wa Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi

*Prof. Shemdoe asema ukusanyaji maoni kwa wadau wa Uvuvi utaondoa malalamiko*

**Na, Stanley Brayton - Dodoma**

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeanza kufanyia kazi maoni mbalimbali yaliyotolewa na wadau wa Sekta ya Uvuvi ili kufanyia marekebisho Mwongozo wa Kitaifa wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi kwa lengo la kukuza tasnia hiyo.

Akizungumza, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Februari 05, 2025 Mkoani Dodoma katika Mkutano wa kupitia Rasimu ya Mwongozo wa Vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi, Prof. Riziki Shemdoe alisema kuwa mwongozo wa awali ulifanyika vyema kiasi cha kupelekea kuwepo na maboresho ya mwongozo huo.

“Timu ya wataalam ilienda kutafuta maoni ambayo yalitoka kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Uvuvi na mpango huu ulifanyika kwa kuzingatia wadau hao waliopo kila mahali hususan wavuvi na imeleta matokeo ambayo tunayaona hapa kwa kuandaliwa mpango huu na kufanyiwa uchambuzi.” alisema Prof. Shemdoe.

Aidha, Prof. Shemdoe alisema huu ukusanyaji wa maoni ni hatua nzuri kwa maana kwamba chochote kitakachoridhiwa katika mwongozo ambao utapitishwa, hakutakuwa na kundi lolote litakalolalamika kuwa halijashirikishwa kwenye mchakato huo kwa sababu maoni yao yote yatakuwepo kwenye mpango huo.

Pia, Prof. Shemdoe alisema viongozi kuomba maoni kwa wadau wa Sekta ya Uvuvi ili kufanyia mapitio mpango huu ni jambo jema sana ambalo lilitakiwa kufanyiwa kazi mapema, kwani mchango wa rasilimali za Sekta ya Uvuvi nchini bado mdogo sana na inapaswa kutumika kwa rasilimali ili kuongeza pato la taifa.

Aliongeza kuwa Sekta za Uvuvi haiwezi kuwa bila uwepo wa mipango mizuri ili walau kufikia asilimia 10 katika kuongeza pato la taifa kwani rasilimali za bahari ni nyingi sana.

# MATUKIO KATIKA PICHA

**Ugawaji Boti za kisasa za Uvuvi - Tanga**











# Rais Samia ameweka nguvu kukuza Uchumi wa Buluu - Mnyeti

## Nikutokana na utoaji mikopo ya boti za uvuvi, Vizimba

- *Wadau wa Uchumi wa Buluu wakiadhimisha Wiki ya Bahari Jijini Dar es Salaam Februari 24- 28 mwaka 2025*

**Na, Hamis Hussein - Dar es Salaam**

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan itaendelea kuhamasisha maendeleo ya Uchumi wa Buluu kwa kuimarisha mazingira ya uwekezaji kwenye bahari.

Akizungumza na vyombo vya habari Februari 24, 2025 baada ya kuzindua Wiki ya Bahari iliyofanyika kwa siku tano katika Hoteli ya Ramada jijini Dar es Saalam, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti alisema wavuvi na wananchi kwa ujumla watapatiwa elimu na nyenzo mbalimbali kwa ajili ya kukuza Uchumi wa Buluu kupitia bahari.

“Mhe. Rais ameweka nguvu kubwa kwenye Uchumi wa Buluu kwa kuanza na elimu kwa wavuvi na wananchi wetu, elimu hii itawafanya kujua nini kilichopo kwenye Uchumi wa Buluu” alisema Mhe. Mnyeti

Aliongeza kuwa jitihada anazoendelea kufanya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni pamoja na utoaji wa boti za uvuvi, vizimba na kuwezesha kilimo cha zao la Mwani.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Tanzania (TAFIRI), Dkt. Ismael Kimirei alisema taasisi hiyo itawasaidia wavumbuzi na watafiti kwa kuyachukua matokeo ya utafiti na kuyawekea msingi ili yawe na tija iliyokusudiwa.

Wiki ya Bahari iiliadhishimishwa jijini Dar es Salaam kwa muda wa siku tano kuanzia Februari 24 hadi 28 Mwaka 2025 na kuhusisha wadau wa maendeleo kutoka mataifa mbalimbali.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti (Mb) akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kufungua mkutano wa kimataifa wa kuadhimisha wiki ya Bahari uliofanyika Hoteli ya Ramada Jijini Dar es Salaam Februari 24, 2025.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) Bw. Abdul Mhinte akizungumza kwenye kikao kazi cha kufanya mapitio ya rasimu ya mitaala ya mafunzo ya mifugo kwa vyuo vya kati ambacho kimefanyika ukumbi wa SAT Mkoani Morogoro Februari 7, 2025.

# Uandaaji Mitaala ya Mafunzo ya Mifugo ushirikishe wadau wa kisekta – Mhinte

## Asisitiza mitaala iendane na sera mpya ya elimu kukidhi mahitaji ya soko

**Na, Hamis Hussein - Morogoro**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) Bw. Abdul Mhinte amesema uandaaji wa mitaala kwa ajili ya mafunzo ya mifugo kwa vyuo vya kati ushirikishe wadau wa sekta husika pamoja kuzingatia sera mpya ya elimu na mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 ili kupata mahitaji halisi yanayohitajika kwenye soko la sasa.

Naibu Katibu Mkuu Mhinte alisema hayo Februari 7, 2025 Mkoani Morogoro wakati akifungua kikao kazi cha kufanya mapitio ya rasimu ya mitaala iliyoandaliwa ya mafunzo ya mifugo kwa vyuo vya kati na kutoa wito kwa timu ya wataalam inayoandaa mitaala hiyo kuhakikisha mitaala mipya inayoandaliwa inaendana na sera ya elimu na mafunzo iliyozinduliwa hivi karibuni na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan.

“Mitaala hii ya kisekta inapoandaliwa inatakiwa kufanyika kwa kushirikisha wadau wa ile sekta, kwasababu usipofanya hivyo unaweza kuandaa mitaala ambayo ikifika kwenye matumizi washiriki au watumiaji wake wanaweza kuona mitaala hiyo haijawasaidia, sasa wakati tunatoa maoni ya kuandaa mitaala hii ni muhimu tuzingatie sera yetu mpya ya elimu ” alisema Bw. Mhinte.

Aidha, alisisitiza kuwa mitaala mipya ya mafunzo ya mifugo inayoandaliwa izingatie mabadiliko ya hali ya teknolojia, mambo mbalimbali yanayotokea duniani katika nyanja ya masoko, biashara na uzalishaji.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Idara ya Mafunzo, Utafiti na Huduma za Ugani Dkt. Angello Mwilawa alisema maboresho ya mitaala inayotumika kwa ajili ya mafunzo ya mifugo kwa vyuo vya kati hufanyika kila mara baada ya miaka mitano lengo likiwa ni kuangalia hali ya halisi ya masomo yanayotolewa yanakidhi mahitaji ya soko la sasa.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala ya Mafunzo ya Vyuo vya Mifugo (LITA) Dkt. Pius Mwambene alisema pamoja na mambo mengine rasimu ya mtaala inayoandaliwa imezingatia Sera ya Mifugo ya Mwaka 2006 pamoja na mikakati ya mabadiliko ya sekta ya mifugo ikiwemo program ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT).



# Serikali kutumia Tafiti za Kisayansi kuboresha Mazao ya Uvuvi baharini

**Lengo ni kuzalisha mazao ya bahari mengi na bora kukidhi mahitaji ya soko**

**Na, Hamis Hussein - Dar es salaam**

Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekubaliana na wadau wa maendeleo ya Sekta ya Uvuvi wa Bahari kutoka mataifa mbalimbali kutumia Sayansi na Utafiti kuboresha mbegu ili ziweze kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi yatakayokidhi mahitaji ya soko.

Akizungumza na vyombo vya habari Februari 27, 2025 wakati wa kufunga mkutano wa kuadhimisha Wiki ya Bahari, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Edwin Mhede alisema uboreshaji wa mbegu za viumbe maji utasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi kupitia Bahari.

"Tumekubaliana itumike sayansi kuondokana na mtazamo kwamba kuna kuvuna kwingi kuliko kiasi kilichopo, kwahiyo tumesema hatuna 'Overfishing' badala yake lazima tuboreshe mbegu za viumbe maji ili uzalishaji uwe mkubwa,mwingi na kwa ubora kukidhi mahitaji ya soko" alisema Dkt. Mhede.

Dkt. Mhede aliongeza kuwa serikali inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imekuwa mstari wa mbele kuimarisha Uchumi wa Buluu kwa kutoa mikopo ya nyenzo za uvuvi ikiwemo boti ambazo imeongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi.

Aidha, aliongeza kuwa serikali itaendelea kuwainua wananchi kiuchumi kwa kuwawezesha kupata teknolojia zitakazokidhi mahitaji ya soko.

Wiki ya Bahari ilianza kuadhimishwa Februari 24, 2025 jijini Dar es Salaam na kukutanisha wadau kutoka mataifa mbalimbali ambapo pamoja na mambo mengine wamejadiliana namna ya kuzilinda rasilimali za bahari ili jamii inayohusika na mnyororo mzima wa shughuli za bahari iweze kunufaika na Uchumi wa Buluu.

> *"Tumekubaliana itumike sayansi kuondokana na mtazamo kwamba kuna kuvuna kwingi kuliko kiasi kilichopo,'Overfishing' badala yake lazima tuboreshe mbegu za viumbe maji ili uzalishaji uwe mkubwa, na kwa ubora kukidhi mahitaji ya soko"*
>
> Alisema Dkt. Mhede



# Wananchi 302 wamepatiwa mafunzo ufugaji samaki kwenye vizimba Ziwa Tanganyika

*Majibu ya Serikali kwa Mbunge wa Kigoma mjini Mhe. Ng'enda Bungeni Februari 12, 2025.*

**Na, Hamis Hussein - Dodoma**

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo imeendelea kuwajengea uwezo wa njia bora za ufugaji wa samaki kwenye vizimba wananchi wanaojishughulisha na ufugaji huo ambapo jumla ya wananchi 302 wanaozunguka Ziwa Tanganyika wamepatiwa mafunzo hayo.

Hayo yamesemwa Februari 12, 2025 na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti wakati akijibu swali la Mbunge wa Kigoma mjini Mhe.Kilumbe Shabani Ng'enda lilihoji ni lini wananchi wanaozunguka Ziwa Tanganyika watapatiwa elimu na nyenzo za kuanzishia ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba.

Mhe. Mnyeti alisema Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) imeendelea kugawa nyenzo za ufugaji wa samaki ambapo vizimba 29, vifaranga na chakula cha kukuzia samaki vyenye thamani ya Shilingi Mil. 602 vilitolewa kwa mikopo isiyokuwa na riba kwa wanufaika wa mikoa ya Kigoma, Rukwa na Katavi.



# Washiriki 17 wahitimu mafunzo ya siku 14 uongezaji thamani Zao la Mwani

**Wahimizwa kuwa wabunifu kutangaza bidhaa zao .**

- Washiriki walitembelea mashamba ya wakulima wengine ili kujifunza kwa vitendo uzalishaji wa zao la mwani

Na Maria Mtambalike - FETA , Mwanza

Washiriki 17 wamejengewa uelewa na ujuzi juu ya kilimo cha mwani na uongezaji thamani wa zao hilo kwa lengo la kwenda kufundisha wenzao kwenye vikundi vya kijamii.

Akiwatunuku vyeti washiriki hao, yaliyohitimishwa Februari 10, 2025, FETA – Mbegani, Mkuu wa Mafunzo ya muda mfupi FETA Bw. Anord Mbunda aliwataka washiriki hao wakatumie vizuri ujuzi walioupata katika kujiongezea kipato binafsi na wanakikundi wengine waliokusudiwa.

Aidha, aliwataka washiriki wawe wabunifu katika kutangaza bidhaa zao watakazozitengeneza ili kilimo cha mwani kiweze kuwanufaisha kiuchumi.

Mkuu wa idara ya Ukuzaji Viumbe Maji FETA, Bw. Mashaka Kapagalla alisema waliwapatia washiriki mafunzo ya nadharia na vitendo zaidi pia washiriki walipata fursa ya kutembelea mashamba ya wakulima wengine ili kuweza kupata uzoefu halisi kutoka kwa wakulima na wazalishaji wa bidhaa za mwani waliopo Wilaya ya Bagamoyo, Mkoani Pwani.

Kwa upande wao washiriki waliopatiwa mafunzo hayo walitoa shukran zao za dhati kwa Shirika la OCODE, Stromme Foundation pamoja na FETA kwa kuwapatia mafunzo hayo yenye tija kwao binafsi na jamii kwa ujumla



Washiriki wa Mafunzo ya Kilimo cha Mwani wakiwa kwenye picha ya pamoja baada ya mafunzo ya kuongeza thamani ya zao hilo yaliyoendeshwa na Shirika la OCODE, Stromme Foundation na Wakala ya Elimu ya Mafunzo ya Uvuvi (FETA) Februari 10,

# FETA yapokea wataalam 28 kutoka Mataifa 11

## Ugeni ulioratibiwa na shirika la VSO international, wapokelewa na Kaimu Mtendaji Mkuu FETA.

**Na, Maria Mtambalike - FETA, Mwanza**



Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA), Februari 10, 2025 ilipokea ugeni wa wataalam 28 kutoka katika mataifa 11 tofauti kwa lengo la kuangalia miundombinu iliyopo FETA kwa ajili ya kusaidia ukuzaji wa Uchumi wa Buluu nchini.

Ugeni huo ulioratibiwa na Shirika la VSO International umehusisha wageni kutoka mataifa ya Uholanzi, Ureno, Ubelgiji, China, Italia, Ufaransa, Denmark, Liberia, Uganda, USA na Norway ulipokelewa na Kaimu Mtendaji Mkuu wa FETA Bw. Anord Mbunda ambapo alipata nafasi ya kueleza majukumu mbalimbali yanayofanywa na wakala pamoja na idara zake.

Ugeni huo umeahidi kushirikiana na FETA katika nyanja mbalimbali zinazohusu fursa za Uchumi wa Buluu-Tanzania.

Aidha, akitoa neno la shukran kwa niaba ya Mtendaji Mkuu, Msimamizi wa Kitengo cha Masoko Bw. Abubakar Mbadjo alipongeza VSO-International kwa kuitangaza FETA vizuri ndani na nje ya nchi.

Pia, aliwakaribisha tena ili kuendeleza juhudi mbalimbali zinazofanya

# Dkt. Kijaji ashiriki Mkutano wa Mawaziri wa Uvuvi ulioandaliwa na IOC nchini Ushelisheli

*Akutana na Waziri wa Uvuvi, atembelea Bandari ya Uvuvi nchini Ushelisheli*



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji amekutana na kufanya mazungumzo na Waziri Kiongozi na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Buluu wa nchini Ushelisheli Mhe. Jean Ferrari.

Mazungumzo hayo yalifanyika Februari 28, 2025 jijini Victoria, Ushelisheli na yalikuwa ni sehemu ya kuimarisha ushirikiano uliopo baina ya Tanzania na Ushelisheli katika masuala ya Uvuvi.

Baada ya mazungmzo na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Buluu nchini Ushelisheli Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji alishiriki Mkutano wa Tatu wa Mawaziri wa Uvuvi wa Nchi za Ukanda wa Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi uliofanyika Februari 28, 2025. Mkutano huo uliandaliwa na Kamisheni ya Bahari ya Hindi (Indian Ocean Commission - IOC) na umewakutanisha Mawaziri kutoka Nchi Tisa za Ukanda huo ikiwemo Tanzania, Ushelisheli,Mauritius, Comoro, Madagascar, Kenya, Msumbiji, Somalia na Reunion.



# MATUKIO KWENYE PICHA

**Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Mhe. Judith Tuluka akisindikizwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji katika Uwanja wa ndege wa Julius Nyerere baada kumalizika kwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za SADC na EAC uliofanyika Ikulu Jijini Dar es Saalam Februari 8, 2025.**









# MATUKIO KWENYE PICHA

Wataalamu, wadau wa Sekta ya Uvuvi na timu ya Mshauri Mwelekezi anayefanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Uvuvi ya Bagamoyo, waliposhiriki kikao cha kupokea taarifa ya upembuzi yakinifu kilichofanyika Februari 04, 2025 Makao Makuu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi yaliyopo Mji wa Serikali Mtumba Dodoma. Baada ya kikao hicho, Mkurugenzi wa Uendelezaji Miundombinu Mhandisi George Kwandu alisaini hati za Ushirikiano na Mtendaji Mkuu wa Kamuni ya Uhandisi ya nchini Korea Bw, Lee Kwang Ho.




Mkurugenzi wa Idara ya Uendelezaji miundombinu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mhandisi George Kwandu akisaini hati za ushirikiano baina ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Kampuni ya Uhandisi ya Dohwa ya nchini Korea kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo Bw. Lee Kwang Ho, Februari 04, 2025 jijini Dodoma.






# MATUKIO KWENYE PICHA

**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji aliposhiriki Mkutano wa Tatu wa Mawaziri wa Uvuvi wa Nchi za Ukanda wa Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi uliofanyika Februari 28, 2025, nchini Ushelisheli. Awali alikutana na kufanya mazungumzo na Waziri Kiongozi na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Buluu wa nchini Ushelisheli Mhe. Jean Ferrari mazungumzo .**














# MATUKIO KWENYE PICHA

**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti (katikati) akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Wiki ya Bahari iliyofanyika kwa siku tano jijini Dar es Salaam kuanzia Februari 24 hadi 28, 2025.**





**Wakurugenzi na Wataalam waliposhiriki shughuli mbalimbali za Wizara ikiwa ni pamoja na ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na serikali ili kuona maendeleo yake.**











# Jarida la Mtandaoni

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
Wizara ya Mifugo na Uvuvi
S.L.P 2870
Mji wa Serikali Mtumba
Dodoma , Tanzania
simu : +255 26 2322610
Barua Pepe : barua@mifugo.go.tz

@wizara ya Mifugo na Uvuvi